TANGAZO LA SERIKALI NA. 247 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MGENDELA NA KIHESA YA MWAKA 2023.

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Mgendela ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Kuandaa na kuhifadhi Mipango ya jumla na kina

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Mji wa Njombe

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Mpaka unaanzia kwenye makutano ya mto Ruhuji na barabara ya mtaa kwenye majira – nukta 694930.3707MS, 8969043.4724KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki kwa umbali wa kilomita 1.102 hadi kwenye majira – nukta 695764.7472MS, 8968323.5771KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.337 hadi kwenye majira – nukta 696101.3046MS, 8968300.9256KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.654 hadi kwenye tawi la mto Ruhuji kwenye majira - nukta 696125.3933MS, 8967647.7051KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi kwa kufuata tawi la mto Ruhuji kwa umbali wa kilomita 0.782 hadi kwenye makutano ya barabara ya mtaa na tawi la mto Ruhuji kwenye majira - nukta 695419.9831MS, 8967310.6857KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wakilomita 0.244 hadi zinapokuta na barabara mbili za mtaa kwenye majira – nukta 695533.491MS, 8967526.0732KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wa kilomita 0.685 hadi kwenye majira – nukta 694868.5465MS, 8967689.5412KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wa kilomita 0.405 hadi kwenye majira – nukta 694776.1369MS, 8967295.1079NKZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.085 hadi kwenye majira – nukta 694691.3801MS, 8967306.3799KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.057 hadi kwenye majira – nukta 694679.465 MS, 8967250.3729 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.054 hadi kwenye majira – nukta 694627.5002 MS, 8967263.7648 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wakilomita 0.655 hadi kwenye majira – nukta 694747.8366 MS, 8967906.3177 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini – Magharibi kwa kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wa kilomita 0.54 hadi zinapokuta na barabara ya Mgendelana bonde kwenye majira – nukta 694350.7027 MS, 8968082.5049 KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata bonde kwa umbali wa kilomita 1.13 hadi ulipoanzia".

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*